OFISI YA RAIS - TAMISSEMI

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA

SHULE YA SEKONDARI MAKOKO (KUTWA) S. L. P. 1095, MUSOMA

# MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE KWA MWAKA 2021

JINA LA MWANAFUNZI: ..................................................................................................................

UTANGULIZI

1:1. Pongezi: Ninafuraha kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na masomo ya Sekondari kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Makoko.

1:2. **Sura ya Shule: Shule** hii ni ya kutwa na mchanganyiko yenye mchepuo wa **sanaa na sayansi** Shule iko mkabala na Seminari ya Makoko jirani na kambi ya Jeshi la **Wananchi Makoko.**

1:3. **Ratiba ya masomo**: Ratiba ya Shule itaanza kila siku saa 1:00 asubuhi hadi saa 9:30 mchana kwa siku za masomo. Masomo yanayofundishwa ni Tisa (9).

1:4. **Kuripoti Shuleni**: Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021**. Na masomo yataanza mara moja.
Wanafunzi wote waripoti wakiwa na wazazi/walezi wao.

2:0. ***Mambo muhimu ya kuzingatia.***

2:1. **Sare ya Shule.**

a) Wavulana wawe na suruali nyeusi 02 zisizobana au model zenye upana wa chini inchi 15,16 au 17, shati tetron nyeupe za kung'aa 02 zenye mikono mifupi, mkanda mweusi wa ngozi wa suruali, viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba na kisigino kifupi, soksi nyeusi jozi 02, tai ndefu nyeusi, sweta ya bluu yenye V shingoni na vesti nyeupe.

b) Wasichana wawe na sketi nyeusi 02 zenye marinda ya kawaida siyo linda box na ziache nchi 04 kufikia kisigino, shati tetroni nyeupe 02 zenye mikono mifupi, viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba na visigino vifupi, soksi nyeupe jozi 02 tai nyeusi ndefu, sweta ya bluu yenye V shingoni.

c) **Nguo za michezo:**

Kila mwanafunzi awe na**T-shirt ya njanoisiyokuwa na michirizi, Bukuta nyekundu au suruali ya traka blue kwa wasichana na raba rangi yoyote.** Nguo hizi zinavaliwa wakati wa michezo tu na zitakaguliwa siku ya kuriport shuleni zije zikiwa kwenye begi la daftari.

Kila mwanafunzi awe na daftari za kutosha (**counter book quire 2** ), bofa, kalamu, mfuko au begi la kubebea daftari, **faili folder 01 na picha passport size 04**, pamoja na vifaa vifuatavyo vya kujifunzia dictionary na **Brighter grammer vol. 1 and 2** kwa ajili ya kujipatia ufahamu wa lugha ya Kiingereza.

2:3. Chakula au chai, nauli ya daladala au baiskeli ni jukumu la mzazi/mlezi shule haitahusika kwa namna yoyote.

2:4. Hijabu kwa wanafunzi Waislam – rangi ifanane na sare za Shule (majumba yavuke kiwiko cha mkono na sketi zifanane na za wengine)

2:5. Mahitaji mengine ya binadamu:
Mzazi/mlezi awasiliane na Shule endapo kuna haja hiyo.

3:0. Sheria na kanuni muhimu za shule hii.

3:1. Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978 na marekebisho yake ya sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Hivyo unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo.

a) Heshima na utii kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba iliyopo Shule ni lazima.

c) Kushiriki katika michezo na gwaride – parade assembly ikiwa ni pamoja na nyimbo za Kitaifa na Shule ni lazima.

d) Kuwahi na kuhusika na shughuli za Shule na nyinginezo utakazo pewa.

e) Ni marufuku mwanafunzi kuwa nje ya mipaka ya Shule bila ruhusa.

f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya Shule, nywele za wanafunzi zitakuwa fupi wakati wote.

g) Kuvaa sare za Shule wakati wote zinapotakiwa.

h) Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote.

i) Kutunza mazingira na mali ya umma.

3:2. **Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa Shule.**

a. Wizi
b. Uasherati
c. Ubakaji
d. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e. Kupigana au kupiga.
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma/Shule.
g. Kudharau Bendera ya Taifa au Gwaride rasmi – parade assembly.
h. Kuoa au kuolewa.
i. Kutoa mimba.
j. Kugoma, kuchochea migomo, kuongoza migomo, kushiriki kuvuruga amani na usalama wa Shule au jamii.
k. Kukataa adhabu.
l. Kuwa na simu ya mkononi, Redio, kamera au silaha yoyote, kutoroka Shuleni, utoro uliokithiri na kwenda nje ya Shule bila kibali.

Tafadhali soma kwa makini na zingatia kikamilifu maagizo haya.

**Mfano wa mavazi yanayotakiwa kuvaliwa kwa wanafunzi wa kike na kiume**

.............................................................................

MKUU WA SHULE

HALMASHAURI YA MANISPAA – MUSOMA

SHULE YA SEKONDARI MAKOKO, S. L. P. 1095 MUSOMA

# FOMU MAALUMU YA MKATABA WA KUTOJIHUSISHA NA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.

## I. TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI:

Jina kamili ........................................................................... jinsi (me/ke)..................... tarehe ya kuzaliwa (ambatanisha nakala aya cheti cha kuzaliwa kama unacho) ........................................ Mahali unapoishi (Kata/Kijiji/Mtaa) ................................................ Uraia ni Mtanzania/Sio Mtanzania .................................. Shule uliyotokea ..................................... Dini/Dhehebu lako ........................................................... kabila ..................................................

## II. TAARIFA YA MZAZI/MLEZI.

Jina kamili ..................................................................... kazi yake .......................... anuani ya makazi ............................................. simu ya mkononi ...................................... Ndugu jamaa wa karibu Atakayetambuliwa na Shule endapo mzazi/mlezi hayupo .............................................................. Na ..............................................................(picha za jamaa hao zitabandikwa kwenye form hii)

## III. KIAPO CHA UTII KWA MWANAFUNZI:

- Mimi (majina kamili) ...........................................................................................
  Nimesoma na kuelewa maelekezo yote juu ya kujiunga na Shule ya Sekondari Makoko. Ninaahidi kwamba nitakuwa mtiifu na mwenye tabia njema na nidhamu bora wakati wote ndani na nje ya Shule. Kwamba nitawaheshimu watu wote na kuwa mfano bora katika kutekeleza sheria, taratibu na kanuni za Shule.
- Hivyo ninaapa kusoma kwa bidii na kutenda kazi zote kwa juhudi na maarifa, sitashiriki katika vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu kama migomo, fujo au kutumia lugha mbaya/chafu na nitakuwa tayari kupokea adhabu yoyote endapo nitapatikana na kosa lolote.

  Sahihi ........................................................... tarehe ..................................................

## IV. AHADI YA MZAZI/MLEZI:

Mimi (majina kamili) ............................................................................................................

Ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi tajwa ninaahidi kushirikiana kwa karibu na walimu na uongozi wa Shule katika malezi ya mwanangu kwa muda wote. Natambua kwamba ninao wajibu muhimu katika kufanikisha maendeleo ya taaluma ya mwanangu. Hivyo nitakuwa tayari kupokea maelekezo yote yatakayotolewa na Shule kuhusu mwanangu au maendeleo ya Shule kuzingatia taratibu zitakazowekwa.

Jina ........................................................................... Sahihi ............................................

## V. UTHIBITISHO:

Imethibitishwa na mimi (majina) .........................................................................

Cheo ..................................................... Sahihi ............................... Tarehe ................................

Muhuri

(Tafadhali ithibitishwe na Afisa Mtendaji wa Mtaa/Kata anayoishi mwanafunzi)

PRESIDENT'S OFFICE - RALG

MAKOKO DAY SECONDARY SCHOOL, P. O. BOX 1095, MUSOMA.

# THE MEDICAL EXAMINATION REQUEST FORM.

(TO BE COMPLETED BY GOVERNMENT MEDICAL OFFICER)

DATE: ............................

A: PART

RE: EXAMINATION TO MR/MISS ..........................................................................................................

AS TO HIS/HER PHYSICAL AND MENTAL FITNESS:

I hereby confirm that I have examined the above named persons' health status in the following categories:

| | | | |
|---|---|---|---|
| I. | Eye sight ............................................ | VI. | Pregnancy ............................................ |
| II. | Hearing ............................................ | VII. | Tuberculosis (TB) .................................. |
| III. | Speech ............................................ | VIII. | Blood Test ........................................ |
| IV. | Epilepsy............................................ | IX. | Venereal Diseases ............................... |
| V. | Leprosy ............................................ | X. | Other serious Diseases ....................... |

PART B:

I therefore consider that he/she is physically and mentally fit/unfit. I also recommend that he/she be given the following treatment/medication before is enrolled as a secondary school student:

i. ..........................................................................................................................

ii. ..........................................................................................................................

PART C:

I suggest that he/she will be ABLE/ not be ABLE; to perform any DUTIES at school for all tires/for at least (state days or months) ...........................................................................................

SEAL:

Signed: ...........................................................................

Official stamp: ..................................................................

NB: - Delete the underlined if not applicable.

- This form is to be submitted dully filled when reporting to school.